JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

MKUU WA TAKUKURU (M)
BARABARA BOMBO HOSPITALI
S.L.P. 1953,
Simu Nambari: 027-2645186,
Nukushi: 027-2647885
Barua Pepe: *rbctanga@pccb.go.tz*
Wavuti: www.pccb.go.tz
21105 TANZANIA

TAARIFA KWA UMMA

UTENDAJI KAZI WA TAKUKURU MKOA WA TANGA KWA KIPINDI CHA MWEZI JANUARI HADI MACHI 2020

Ndugu Waandishi wa Habari,

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Tanga, tumeendelea na utekelezaji wa majukumu yetu ya kusimamia, kuratibu na kuongoza Mapambano Dhidi ya Rushwa kwa kuchukua hatua zinazofaa kwa lengo la Kuzuia na Kupambana na vitendo vya rushwa katika idara za Serikali, mashirika ya umma na taasisi binafsi mkoani Tanga kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya mwaka 2007 (pamoja na kanuni zake za mwaka 2009).

Kwa kipindi cha **mwezi Januari hadi Machi 2020** ofisi ilifanya kazi katika maeneo ya Uchunguzi na Mashitaka, Udhibiti wa Mianya ya Rushwa pamoja na Elimu kwa Umma kama ifuatavyo:

1. UCHUNGUZI NA MASHITAKA.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Katika Uchunguzi, TAKUKURU Mkoa wa Tanga imepokea jumla ya taarifa **133** za vitendo vya rushwa. Mchanganuo wa taarifa hizo kwa kipindi tajwa kiidara na idadi ya malalamiko ni kama ifuatavyo;- Serikali za Mitaa (Halmshauri za wilaya/Jiji) **25**, Ardhi **12**, Polisi **11**,Mahakama **10**, Elimu **9,** Afya **9,** TAMISEMI **8,** Vyama vya ushirika **7,** Biashara **6,** Tanesco **6,** Siasa **5,** Baraza la Ardhi **4**, Kilimo **3**, Uchaguzi wa Serikali za mitaa **3**, Misitu **3 ,** Maji **2,** NIDA **2,** Uvuvi **2,** Maji **1**, Usafirishaji 1, Mifugo **1** na NIMRI **1** na Taarifa binafsi **2** Kati ya taarifa hizo zilizopokelewa, taarifa **33** zinaendelea kuchunguzwa na TAKUKURU taarifa **97** zimefungwa na ushauri kutolewa kwa watoa taarifa kwani wengi wao wamefika kupata ushauri na wengine kuelekezwa mahala husika kutokana na taarifa zao **na** taarifa **3** zimehamishiwa Idara nyingine ili waweze kuzifanyia kazi kwa mujibu wa sheria zao.

Kwa upande wa uendeshaji mashtaka, TAKUKURU Mkoa wa Tanga kwa kipindi cha mwezi wa Januari hadi Machi 2020, imeendesha jumla mashauri **22** mahakamani ambapo mashauri **19** kati ya hayo ni yale yaliyofunguliwa katika kipindi cha nyuma kabla ya Januari 2020 na mashauri **4** yamefunguliwa katika kipindi cha Januari - Machi 2020.

Katika kipindi hicho jumla ya mashauri 4 yaliyokuwa yakiendeshwa Mahakamani yalimalizika ambapo Jamhuri imeshinda matatu na moja mshtakiwa ameachiwa huru. Mashauri hayo ni pamoja na shauri Na. CC.08/2020 la Pangani mshatakiwa alihukumiwa kifungo cha miaka mitatu jela au faini ya Shilingi laki tano (500,000/=) na amelipa faini kukwepa kifungo;

Shauri Na. CC.01/2018 la Handeni mshatakiwa alihukumiwa kifungo cha miaka minne jela au faini ya Shilingi Milioni moja (1,000,000/=) na amelipa faini akawepa kwenda jela; shauri Na. CC.01/2020 la Kilindi mshatakiwa alihukumiwa kifungo cha miaka mitatu jela au faini ya Shilingi laki tano (500,000/=) na amelipa faini kukwepa kifungo; na pia shauri Na. CC.01/2019 la Wilaya ya Kilindi, usikilizwaji wake umekamilika na mtuhumiwa aliachiwa huru kwa kuwa hakuwa na kesi ya kujibu.

2. UZUIAJI RUSHWA:

(a) Uchambuzi wa Mifumo:

TAKUKURU Mkoa wa Tanga, Kupitia Dawati la Uzuiaji Rushwa, kwa kipindi cha mwezi Januari, 2020 hadi Machi, 2020 imeendelea kufanya kazi mbalimbali zinazolenga kudhibiti mianya ya rushwa katika sekta mbalimbali. Miongoni mwa kazi zilizofanyika ni pamoja na kazi ya Uchambuzi wa mifumo **7** katika maeneo mbalimbali ambayo ni Halmashauri, Vyama vya Ushirika na Uhifadhi wa wanyama pori. Chambuzi hizo za mifumo zilifuatiwa na warsha/ vikao **2** pamoja na kazi **4** za Ufuatiliaji wa maazimio yanayotokana na warsha mbalimbali zilizofanyika katika kipindi tajwa.

(b) Ufuatiliaji wa Miradi ya Maendeleo

Katika kipindi cha Januari hadi Machi, 2020 TAKUKURU (M) Tanga imeendelea kufanya ufuatiliaji wa matumizi sahihi ya fedha zinazoletwa na Serikali ili kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwa ni pamoja na miradi ya Afya, Maji, Ujenzi wa majengo mbalimbali ya umma na barabara pamoja na Elimu katika eneo la ujenzi wa madarasa na umaliziaji wa maboma katika shule mbalimbali za sekondari Mkoani Tanga.

Katika kipindi tajwa TAKUKURU Tanga imefanya ufuatiliaji wa miradi **16** ya maendeleo ambayo thamani yake kwa ujumla inafikia Shilingi Bilioni tatu, milioni mia moja kumi na saba na arobaini na tano elfu, mia saba na mbili na senti hamsini tu. (**TShs. 3,117,045,702.50**). Kazi ya ufuatiliaji wa miradi hiyo inaendelea kufanyika kwani baadhi ya miradi haijakamilika na baadhi inaonekana kuwa na kasoro.

FEDHA ZILIZOOKOLEWA KUTOKANA NA KAZI ZA UCHUNGUZI NA UDHIBITI.

Katika utekelezaji wa majukumu yake ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa TAKUKURU Mkoa wa Tanga imefanikiwa kuokoa fedha taslimu kiasi cha Shilingi Milioni tatu laki sita na sitini na nane elfu (**Shs 3,668,000/=)** ambazo zilikuwa zimetumika ama kuchukuliwa kinyume na Sheria, kanuni na taratibu sahihi za matumizi ya fedha za umma pamoja na kudhibiti kiasi cha Shilingi Milioni kumi na tano laki tatu na tisini elfu(**Shs 15,390,000**).

Aidha katika kipindi hicho TAKUKURU tumefanikiwa pia kudhibiti kiasi cha Shilingi 1,794,000/= zilizotokana na kukamata mbao ambazo zilivunwa bila ya kibali cha Serikali ya Kijiji cha Mseko katika Wilaya ya Pangani.

(c) ELIMU KWA UMMA

Katika jukumu la kuelimisha, kuhamasisha na kushirikisha Umma katika Mapambano Dhidi ya Rushwa, kwa kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Machi mwaka 2020 TAKUKURU Mkoa wa Tanga imefanya; uimarishaji wa klabu za kupambana na rushwa **148** katika shule za msingi, sekondari na vyuo mbalimbali na tumefungua klabu mpya **13**. Pia tumeendesha mikutano ya hadhara **80**, semina **26**, vipindi vya redio **43 na** kuandaa makala **20** pamoja na kufanya onyesho **01.** Makundi mbalimbali ya wananchi wakiwemo watumishi wa umma, wanafunzi na wafanyakazi wa mashirika mbalimbali wameweza kufikiwa.

(d) HITIMISHO

Ndugu Waandishi wa Habari,

TAKUKURU Mkoa wa Tanga katika kipindi cha mwezi April hadi Juni mwaka 2020 tunategemea tutaendelea kutoa elimu na kuwahamasisha wananchi waongeze ushiriki wao katika mapambano haya dhidi ya Rushwa kwa kufichua vitendo vyote vinavyoashiria uwepo wa Rushwa **(kutegemea na kumalizika maambukizi ya ugonjwa wa Korona)**.

Aidha tutaendelea kutoa elimu juu ya Rushwa wakati wa uchaguzi ili kuhakikisha matukio yote yanayohusu vitendo vya Rushwa kabla, wakati na baada ya uchaguzi yanaripotiwa na kuchukuliwa hatua stahiki. TAKUKURU Mkoa wa Tanga tutaendelea pia na kazi ya kufatilia urejeshwaji wa fedha za madeni ya vyama vya ushirika na pia miradi ya maendeleo ili maendeleo ya kweli ya wananchi yaliyokusudiwa na Serikali yetu yaweze kupatikana.

Ni jukumu la kila Mtanzania kuendelea kushiriki katika mapambano dhidi ya Rushwa pasipo kuoneana aibu kwani athari ya rushwa ni ya taifa zima.

TAKUKURU Mkoa wa Tanga inaendelea kutoa wito na kuwakaribisha wananchi na wadau wote wa Mapambano Dhidi ya Rushwa kufika ofisi zetu kutoa taarifa kwa njia yoyote watakayo ona mwafaka kwao. Mwananchi au mdau yeyote anaweza kuwa siliana moja kwa moja na viongozi wa TAKUKURU Mkoa wa Tanga ni kwa namba zifuatazo:-

- 0689-797-998 na 0738-150-225(Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Tanga)
- 0784-280-663 na 0738-150-228 (Mkuu wa TAKUKURU Wilaya ya Kilindi)
- 0782-208-008 na 0738-150-232 (Mkuu wa TAKUKURU Wilaya ya Muheza)
- 0784-290-117 na 0738-150-230 (Mkuu wa TAKUKURU Wilaya ya Lushoto)
- 0786-207-311 na 0738-150-233 (Mkuu wa TAKUKURU Wilaya ya Pangani)
- 0782-866-867 na 0738-150-231(Mkuu wa TAKUKURU Wilaya ya Mkinga)
- 0713-442-425 na 0738-150-229 (Mkuu wa TAKUKURU Wilaya ya Korogwe)
- 0688-313-853 na 0738-150-227 (Mkuu wa TAKUKURU Wilaya ya Handeni)

Pia mtoa taarifa aneweza kupiga simu ya Bure 113 au ukatuma ujumbe mfupi wa maandishi kwa kupiga *113# na kufuata maelekezo.

Imetolewa na Dkt. Sharifa Bungala - Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa TANGA.
April 17, 2020